**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**

# TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA MAMBO YA NJE, NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018; PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019

Ofisi ya Bunge,
S. L. P 941,
**DODOMA**

Mei, 2018.

# A. YALIYOMO

**SEHEMU YA KWANZA** .......................................................... I
1.0 UTANGULIZI .......................................................... i
**SEHEMU YA PILI** .......................................................... III
2.0 MAPITIO YA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018 .......................................... iii
2.1 Uzingatiaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati .......................... iii
2.2 Uchambuzi wa Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 .......................................... v
2.2.1 Ukusanyaji wa maduhuli .......................................... **v**
2.2.2 Upatikanaji wa fedha kutoka Hazina .............................. **vi**
**SURA YA TATU** .......................................................... VII
3.0 UCHAMBUZI WA MPANGO NA BAJETI YA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019 .. vii
3.1 Uchambuzi wa Malengo ya Bajeti .................................. vii
3.2 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato .............................. viii
3.3 Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi .............................. ix
**SURA YA NNE** .......................................................... XII
4.0 MAONI NA USHAURI .......................................................... xii
**SURA YA TANO** .......................................................... xviii
5.0 HITIMISHO .......................................................... xviii

## SEHEMU YA KWANZA

## UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, [Kanuni za Bunge], naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Mambo ya Nje, na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018; pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019, na kuliomba Bunge lako tukufu liipokee taarifa hii na kuikubali, kisha kuidhinisha Bajeti ya Wizara hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kifungu cha 6 (3) cha Nyongeza ya Nane, ya Kanuni za Bunge, Wizara hii ni mojawapo ya Wizara inayosimamiwa na Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama. Aidha, Kifungu cha 7 (1) (a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge kimezipa jukumu Kamati za Kisekta ikiwemo Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, kushughulikia Bajeti za Wizara inazozisimamia. Naomba kulijulisha Bunge lako tukufu kuwa katika kutekeleza jukumu hilo, Kamati ilikutana na Waziri wa Mambo ya Nje, na Ushirikiano wa Afrika Mashariki tarehe 23 na 26 Machi, 2018.

**Mheshimiwa Spika**, katika kikao hicho, Kamati ilipokea Taarifa ya Wizara kuhusu utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 kama inavyoelekeza Kanuni ya 98 (2) ya Kanuni za Bunge kwa lengo la kulinganisha na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii, kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

**Mheshimiwa Spika**, ili kulisaidia Bunge lako Tukufu kufuatilia ipasavyo utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018, pamoja na kuishauri vema Serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019, Taarifa ninayoiwasilisha inatoa maelezo kuhusu:-

i) Mapitio ya Taarifa ya Wizara kuhusu uzingatiaji wa maoni yaliyotolewa na Kamati Bungeni wakati wa kujadili Bajeti ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018;
ii) Uchambuzi wa ukusanyaji wa maduhuli ikilinganishwa na lengo lililowekwa kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018;
iii) Mapitio ya Taarifa ya Wizara kuhusu upatikanaji wa fedha zilizoidhinishwa na Bunge pamoja na utekelezaji wa majukumu na malengo ya bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018;
iv) Uchambuzi wa majukumu na malengo yanayowekwa kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019;
v) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019; na
vi) Mapitio ya Malengo ya bajeti na Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

**Mheshimiwa Spika**, lengo ni kuliwezesha Bunge kupata taswira ya hali ya utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 na kulinganisha na Makadirio ya fedha za matumizi yaliyowasilishwa na mtoa hoja mapema leo ili Bunge liweze kujadili na kuamua kuhusu Maombi ya Wizara hii.

## SEHEMU YA PILI

## MAPITIO YA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa ya Utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 ilihusu maeneo makuu mawili. Maeneo hayo ni Uzingatiaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati na Mapitio ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge. Naomba kulijulisha Bunge hili kuwa, Kamati ilipitia na kuchambua kwa kina mambo yote mawili kama ifuatavyo:-

### Uzingatiaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati

**Mheshimiwa Spika**, tutakumbuka kuwa Bunge hili lilipokuwa linajadili hoja ya Serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018, Kamati ilitoa ushauri katika jumla ya mambo makuu kumi na tano katika kufuatilia uzingatiaji wa ushauri huo, tarehe 23 Machi, 2018 Waziri wa Mambo ya Nje, na Ushirikiano wa Afrika Mashariki aliijulisha Kamati kuhusu utekelezaji wa ushauri huo. Naomba kulijulisha Bunge kwamba upo ushauri uliozingatiwa, upo unaoendelea kuzingatiwa na upo ushauri uliopewa uzito kidogo katika utekelezaji.

**Mheshimiwa Spika**, miongoni mwa ushauri uliozingatiwa ni kuhusu ufunguzi wa Ofisi za ubalozi au Balozi za heshima katika nchi zenye uhusiano mkubwa wa kibiashara na Tanzania kama vile Lubumbashi DRC, Cuba na Guangzhou – China. Maelezo ya Waziri yalionesha kuwa kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019, Serikali imetenga shilingi 9,329,800,000/= kwa ajili ya kufungua ubalozi mpya Cuba na Konseli kuu katika miji ya Lubumbashi – Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na Guangzhou – China. Kamati

inaipongeza Serikali kwa hatua hiyo inayoweza kuinufaisha nchi yetu kutokana na fursa mpya za kiuchumi na kibiashara.

**Mheshimiwa Spika**, ushauri unaoendelea kufanyiwa kazi na ambao utekelezaji wake haujaanza ni pamoja na ujenzi wa Ofisi ya Wizara kwa upande wa Zanzibar. Naomba kulikumbusha Bunge lako tukufu kuwa, tarehe 31 Mei, 2017 wakati wa kujadili Bajeti ya Wizara hii, Kamati ilishauri kwamba Serikali ifanye matengenezo makubwa au kujenga jengo jipya la Ofisi ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki huko Zanzibar. Hadi kufikia tarehe 23 Machi, 2018 wakati Kamati ilipochambua Taarifa ya Wizara hii, hakuna ukarabati wa jengo hilo au ujenzi wa jengo jipya kwa madhumuni hayo, uliokuwa umepangwa.

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa ya Waziri ilionesha kuwa bado mazungumzo yanaendelea baina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu umiliki wa jengo linalotumiwa hivi sasa na Idara ya Mambo ya Nje Zanzibar. Ahadi iliyotolewa ni kwamba, mazungumzo yatakapokamilika na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikipatiwa umiliki wa jengo husika, ukarabati utaanza mara moja. Ni maoni ya Kamati kuwa kasi ya kufanikisha mazungumzo hayo inapaswa kuongezwa na njia ya kujenga jengo lingine inaweza kutumika iwapo mazungumzo hayo hayatafanikisha azma ya Wizara.

**Mheshimiwa Spika**, kwa ujumla ushauri wa Kamati umefanyiwa kazi na uzingatiaji upo katika hatua mbalimbali. Hata hivyo, Kamati inasisitiza kuwa, kwa mambo ambayo uzingatiaji wake haujafikia hatua kubwa, ushauri wa Kamati unapaswa kupewa

uzito stahiki. Kwa mfano, suala la kukamilisha Sera mpya ya Mambo ya Nje, inayopaswa kutoa dira na mwelekeo unaoendana na hali ya kisasa ya Diplomasia ya Uchumi duniani, linapaswa kupewa uzito mkubwa zaidi kuliko ilivyo sasa.

**Mheshimiwa Spika**, Naomba kulijulisha Bunge lako tukufu kuwa Taarifa iliyotolewa kwenye Kamati inaonesha kuwa hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa Rasimu ya Sera. Aidha, hatua inayofuata na ambayo haijaanza ni kuandaa mkakati wa utekelezaji wa Sera iwapo itapitishwa ndani ya Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, imepita takribani miaka kumi na saba sasa tangu Sera iliyopo ilipotungwa. Wakati huo Wizara haikuwa na jukumu la kushughulikia au kuratibu masuala ya mtangamano wa Afrika Mashariki. Kamati ina maoni kuwa kuna umuhimu mkubwa wa kuongeza kasi ya kukamilisha mchakato wa Sera hii na mkakati wake ili kuikamilisha kabla ya Mwaka wa Fedha 2019/2020.

## Uchambuzi wa Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipitia Taarifa ya utekelezaji wa Bajeti kwa kuchambua hali ya ukusanyaji wa mapato hadi mwezi Februari 2018 pamoja na upatikanaji wa fedha kutoka Hazina kwa kipindi cha Julai, 2018 hadi tarehe 20 Machi, 2018.

## Ukusanyaji wa maduhuli

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 Wizara hii ilikuwa na lengo la kukusanya maduhuli ya Serikali kiasi cha

shilingi **25,773,820,000/=**. Hata hivyo, Kamati ilijulishwa kuwa hadi kufikia mwezi Februari, 2018, Wizara ilikusanya Jumla ya shilingi **18,665,002,685.57/=** sawa na **asilimia 72.4** ya lengo la ukusanyaji.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifanya ulinganisho wa hali ya ukusanyaji kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 hadi kufikia Februari, 2017. Naomba kulijulisha Bunge lako tukufu kuwa katika kipindi cha Julai 2016 hadi Februari, 2017 makusanyo yalifikia **asilimia 60.7** tofauti na **asilimia 72.4** ya lengo kwa kipindi cha Julai, 2017 hadi Februari, 2018. Kamati ina maoni kwamba mwenendo huu wa ukusanyaji wa maduhuli ulikuwa wa kuridhisha.

**Upatikanaji wa fedha kutoka Hazina**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipochambua Taarifa ya upatikanaji wa fedha kwa mwaka 2017/2018 ilibaini kuwa hadi kufikia tarehe 20 Machi, 2018 Wizara ilipokea **Shilingi 98,617,704,687.20** sawa na **asilimia 65.38** ya Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge lako tukufu. Hali hiyo ni tofauti na Mwaka wa Fedha 2016/2017 ambapo hadi kufikia mwezi Machi, 2017, Wizara ilipokea **Shilingi 87,201,012,183.00** sawa na **asilimia 56** ya Bajeti iliyokuwa imeidhinishwa na Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, kati ya fedha zilizopokelewa katika Mwaka wa Fedha 2017/2018, **Shilingi 88,228,634,384.20** zilikuwa za Matumizi Mengineyo sawa na **asilimia 66** ya **Shilingi 133,424,290,000.00** zilizotengwa, **Shilingi 7,468,874,648.00** kwa ajili ya Mishahara sawa na **asilimia 79** ya Shilingi **9,421,129,000.00** zilizotengwa, na **Shilingi**

**2,920,195,655.00** zilikuwa za Miradi ya Maendeleo sawa na **asilimia 36.5** ya **Shilingi 8,000,000.00** zilizotengwa.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilijulishwa kuwa asilimia kubwa ya fedha zilizopatikana kutoka Hazina ilitumika kugharamia uendeshaji wa Ofisi za Balozi zetu nje ya nchi; safari za Viongozi wa Kitaifa nje ya nchi; ukarabati wa majengo ya Balozi zetu zilizopo Kampala, Kinshasa, Lilongwe na Brussels; pamoja na utekelezaji wa majukumu mengine.

**Mheshimiwa Spika**, Mwelekeo huu wa matumizi hautofautiani sana na mwelekeo ulivyokuwa kwa kipindi cha Julai 2016 hadi Machi, 2017. Hata hivyo, bado kuna umuhimu mkubwa kwa Wizara kupitia vipaumbele vyake kabla ya kuanza matumizi ya fedha zinazopokelewa.

# SURA YA TATU

## UCHAMBUZI WA MPANGO NA BAJETI YA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019

### Uchambuzi wa Malengo ya Bajeti

**Mheshimiwa Spika**, kabla ya kueleza uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019, napenda kutoa Taarifa kwa Bunge lako tukufu kuwa, Kamati ilielezwa Miongozo Kumi na Mbili iliyozingatiwa wakati wa maandalizi ya Bajeti ya Wizara hii.

**Mheshimiwa Spika**, Miongoni mwa miongozo hiyo, ni Sera ya Mambo ya Nje ya mwaka 2001, ambayo ina umri wa takribani miaka kumi na saba. Miongozo mingine ni pamoja na Mpango wa Pili wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/2017 – 2020/21) na Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilielezwa zaidi kuwa Wizara imepanga Malengo Makuu Kumi na Mbili ya Kibajeti kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019. Mfano wa Malengo hayo ni kuandaa Sera ya Taifa ya Diaspora itakayotoa mwongozo wa namna ya kuwashirikisha Diaspora wa Tanzania katika kuchangia maendeleo ya nchi yao. Lengo lingine ni kuratibu na kusimamia majadiliano ya Rasimu ya Andiko la Katiba ya Fungamano la Kisiasa la Afrika Mashariki (*East Africa Political Federation*).

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba hakuna lengo mahsusi la ukamilishaji wa Mapitio ya Sera ya Taifa ya Mambo ya Nje kwa wakati huu, ambapo Wizara itaratibu majadiliano kuhusu Andiko la Katiba ya Fungamano la Kisiasa la Afrika Mashariki. Ni maoni ya Kamati kuwa jambo hili linapaswa kupewa umuhimu kwa kiwango stahiki.

**Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato**

**Mheshimiwa Spika**, katika uchambuzi wa bajeti ya Wizara hii, Kamati ilichambua Makadirio ya ukusanyaji wa Mapato yanayopendekezwa kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 na kubaini kuwa Makadirio hayo yanatofautiana kidogo na lengo lililowekwa kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018. Katika Mwaka wa Fedha unaoisha, Wizara ilikuwa na lengo la kukusanya shilingi **25,773,882,820/-** wakati kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019,

Wizara inalenga kukusanya kiasi cha Shilingi **28,564,154,100/-.** Lengo hili la Makusanyo limeongezeka kwa kiasi cha shilingi **2,790,271,280/-** sawa na **asilimia 10.8.**

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi zaidi ulionesha kuwa ongezeko hilo lipo katika lengo la Makusanyo ya Balozi zetu nje ya nchi ambapo zilikuwa na lengo la kukusanya jumla ya shilingi **25,672,638,700/-** kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 lakini kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 zinapewa lengo la kukusanya jumla ya shilingi **28,448,635,288/-**.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ililinganisha lengo la kukusanya Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 na mwenendo halisi wa ukusanyaji wa Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 ili kutathmini lengo la maduhuli linalopangwa kwa Mwaka wa Fedha unaofuata. Tathmini imeonesha kuwa hadi kufikia Mwezi Februari, 2018 ni kiasi cha Shilingi **18,665,002,685.57 sawa na asilimia 72.70** kilikuwa kimekusanywa. Kwa mwenendo huo, kiasi cha lengo kilichobaki ni shilingi **7,113,591,658.32 sawa na asilimia 27.30** ambacho kinaweza kukusanywa kwa kipindi cha mwezi Machi hadi Juni, 2018. Kwa mwenendo huu, Kamati inaridhika kuwa lengo la Mapato linalowekwa linaendana na hali halisi.

**Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilijulishwa kuwa Wizara hii inaomba kuidhinishiwa kiasi cha shilingi **177,006,232,000/=** ambapo shilingi **154,810,812,000/=** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC), shilingi **11,795,420,000/=** ni kwa ajili ya Mishahara na shilingi **10,400,000,000/=** ni kwa ajili ya kugharamia Miradi ya Maendeleo.


**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifanya Uchambuzi wa maombi hayo na kuona kuwa **87.5%** ya Makadirio hayo ni kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli, **6.7%** ni kwa ajili ya Mishahara na **5.1%** ni kwa ajili ya kugharamia Miradi ya Maendeleo kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 1 na Grafu Na 1 na Na. 2 katika Taarifa hii.

| **MWAKA** | **2017/2018** | | **2018/2019** | | **% ONGEZEKO** |
|---|---|---|---|---|---|
| **AINA YA MATUMIZI** | **KIASI** | **ASILIMIA** | **KIASI** | **ASILIMIA** | |
| ***MISHAHARA (PE)*** | 9,421,129,000.00 | 6.2 | 11,795,400,000.00 | 6.7 | **25.2** |
| ***MATUMIZI MENGINEYO (OC)*** | 133,424,290,000.00 | 88.5 | 154,810,812,000.00 | 87.5 | **16.** |
| ***MIRADI YA MAENDELEO*** | 8,000,000,000.00 | 5.3 | 10,400,000,000.00 | 5.9 | **30** |
| ***JUMLA*** | 150,845,419,000.00 | 100 | 177,006,212,000.00 | 100 | **17.3** |

**Jedwali Na. 01:**

Uwiano wa aina za Bajeti ya Matumizi na ulinganisho wake kwa mwaka 2017/2018 na 2018/2019

**Chanzo: Randama ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Uk. 10 na Uk. 74, Mwezi, Machi, 2018**




**Chanzo**: **Takwimu katika Jedwali Na. 1.**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifanya ulinganisho kati ya Bajeti ya mwaka 2017/2018 na mwaka 2018/2019 kama inavyoelekeza Kanuni ya 98 (2) ya Kanuni za Bunge. Katika ulinganisho huo, Kamati ilibaini kuwa fedha zinazoombwa kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 zimeongezeka kwa **asilimia 17.3** kutoka shilingi **150,845,419,000/=** zilizoidhinishwa Mwaka 2017/2018 hadi shilingi **177,006,212,000/=** zinazoombwa kuidhinishwa na Bunge leo kama ilivyobainishwa katika Jedwali Namba 1.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipochambua zaidi ilibaini kuwa Bajeti ya Mishahara, Bajeti ya Matumizi Mengineyo na Bajeti ya Miradi ya Maendeleo imeongezeka ikilinganishwa na mwaka 2017/2018. Bajeti ya Mishahara imeongezeka kwa **asilimia 25.2,** Bajeti ya Matumizi Mengineyo imeongezeka kwa **asilimia 16** na Bajeti ya Maendeleo kwa **asilimia 30.** Pamoja na hivyo, sura ya uwiano wa Bajeti iliyotengwa kwa vipengele hivyo vitatu kwa Mwaka 2017/2018 na Mwaka 2018/2019 haitofautiani sana kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 1 na Grafu Na. 1 pamoja na Grafu Na. 2



**Mheshimiwa Spika**, Kamati inatambua kuwa mwenendo huu wa uwiano wa Bajeti utaendelezwa na hata kuboreshwa zaidi. Ni imani ya Kamati kuwa hata baada ya kuidhinisha Makadirio haya, upatikanaji wa fedha utakuwa mzuri na unaozingatia namna Bunge linavyoidhinisha Makadirio haya ya Mapato na Matumizi.

# SURA YA NNE

## MAONI NA USHAURI

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia Dhamira ya Wizara ya kusimamia na kutekeleza diplomasia ambayo itachangia katika shughuli za kiuchumi na kuwezesha mageuzi ya haraka na maendeleo endelevu ya Tanzania, Kamati inatoa maoni na ushauri ufuatao:-

i) Serikali ihakikishe fedha zote kiasi cha Shilingi 9,329,800,000.00 ambazo zimetengwa kwa ajili ya kufungua Balozi mpya huko Cuba na Konseli Kuu katika miji ya Lubumbashi- Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na Guangzhou-China zinatolewa kwa wakati na kutumika kama ilivyokusudiwa. Kamati inaamini pesa hizo zikitolewa kwa ukamilifu zitawezesha ufunguzi wa Ubalozi huo na Konseli kuu hizo na hatimaye nchi yetu kunufaika na fursa za kiuchumi na kibiashara. Aidha, Serikali iweke mikakati zaidi ya kufungua Balozi au Balozi za Heshima katika nchi nyingine zinazoendelea kukua kwa kasi kiuchumi.

ii) Kwa kuwa kiwango cha fedha za bajeti zinazotolewa kwa Wizara kimekuwa hakiendani na mtiririko wa Fedha uliopangwa jambo ambalo linasababisha Wizara na Balozi zake kutotekeleza

ipasavyo majukumu yake ya msingi hususana Sera ya Mambo ya Nje inayoweka msisitizo wa Diplomasia ya Uchumi, Serikali ihakikishe kuwa fedha zinazotengwa zinatolewa kwa kuzingatia mtiririko uliopangwa.

iii) Kwa kuwa Kiwanja kilichotolewa na Serikali ya Oman kwa ajili ya kujenga Ubalozi wa Tanzania jijini Muscat hakijaendelezwa tangu kilipowekewa jiwe la Msingi na Rais Mstaafu wa Awamu ya Nne Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete Mwaka 2012, na kwa kuwa upo uwezekano wa Kiwanja hicho kutwaliwa na Serikali ya Nchi hiyo endapo kitaendelea kukaa bila kuendelezwa, Serikali itoe Shilingi 1,894,056,560.00 zilizokuwa zimetengwa katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 kwa ajili ya ujenzi wa jengo la Ubalozi kabla ya Mwaka huu wa Fedha kuisha. Sambamba na ushauri uliotolewa hapo juu, Serikali itoe fedha za Maendeleo zilizotengwa katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 kwa ajili ya ukarabati wa majengo ya Ubalozi wetu wa Cairo, Ukarabati wa miundombinu ya Chuo cha Diplomasia, Dar es Salaam na Ujenzi wa Makazi ya Balozi, Addis Ababa.

iv) Pamoja na kwamba Serikali ilijiwekea Mkakati wa miaka kumi na tano (2001/2003-2016/2017) wa kuendeleza viwanja, kukarabati na kununua majengo ya Ofisi na Makazi ya Watumishi Balozini, Mkakati huo haujatekelezwa kwa kiwango cha kuridhisha. Kamati inaendelea kuishauri Serikali kutoa kipaumbele katika kuendeleza viwanja 12 ambavyo baadhi yake ni vya muda mrefu (Kama vile Viwanja vilivyopo Maputo, London, Adis Ababa, Nairob, Muscat) na kuboresha majengo ya Ofisi na Makazi ya Watumishi katika Balozi zetu ikibidi kwa

kutumia mikopo ya muda mrefu lakini yenye riba nafuu. Hii itasaidia Serikali kuokoa fedha nyingi za walipa kodi zinazotumika kwa ajili ya kukodi majengo ya Ofisi na Makazi katika Balozi zetu nje ya Nchi ambapo kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 Shilingi **21,667,174,191.00** zimetengwa kwa ajili hiyo. Sambamba na hilo, hii itawezesha Serikali kujenga majengo ya kisasa ya Balozi zetu ambayo yakimalizika yataingiza fedha nyingi za kuendesha Balozi hizo na kusitisha utaratibu wa kupanga Ofisi na nyumba za watumishi.

Aidha, Kamati imebaini utaratibu huo ni wenye tija na mafanikio makubwa kama vile inavyoonekana katika Ubalozi wa Maputo – Msumbiji ambako kwa Mwaka ujao wa Fedha wa 2018/2019 hawatahitaji na hawakupangiwa fedha za pango;

v) Kwa kuwa Wizara imekubaliana na ushauri wa Kamati wa kupanga Miradi michache itakayoweza kutekelezwa kwa mwaka na hatimae kuweka Miradi mitatu tu ya Maendeleo kwa Mwaka ujao wa Fedha 2018/2019, Serikali ihakikishe kuwa inaipatia fedha Miradi hiyo hususan ule wa ujenzi wa Ofisi ya Ubalozi wa Muscat – Oman ambako Serikali inaweza kukusanya fedha nyingi za maduhuli kwa miaka ijayo;

vi) Kamati inatambua nia njema ya Serikali katika kuondoa suala la *retention* kwa Wizara zake zote. Hata hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuweka utaratibu maalum utakaoruhusu Balozi zetu nje ya Nchi kubaki na angalau asilimia 40 ya makusanyo yao ili yawawezeshe katika kutekeleza majukumu yao hususan kukarabati majengo ambayo mengi yao yamekaa muda mrefu bila kufanyiwa ukarabati. Aidha, Serikali ione umuhimu wa kuweka

utaratibu maalum wa kuziwesha baadhi ya Balozi kutuma fedha za makusanyo moja kwa moja Serikalini badala ya kupitia katika Ubalozi mwingine ili kuepukana na changamoto ya *exchange losses* ambayo inaathiri kiwango cha mapato yanayokusanywa.

vii) Kwa kuwa baadhi ya Balozi zetu zinakabiliwa na changamoto ya kuwa na watumishi wachache kutokana na baadhi ya watumishi kustaafu na wengine kurejea nyumbani baada ya kumaliza muda wa kufanya kazi Balozini, Serikali ione umuhimu wa kupeleka watumishi zaidi katika Balozi zenye uhitaji ili kuziwezesha kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi. Aidha, kwa kuwa baadhi ya wataalam katika Balozi zetu hawana weledi wa Diplomasia ya Uchumi, Serikali ihakikishe watumishi wanaopelekwa katika Ofisi zetu za Ubalozi wana utaalam, ujuzi na uzoefu "Professionals" kuhusu masuala yanayohusu Diplomasia ya Uchumi, ili kuondoa changamoto za uwajibikaji na utekelezaji wa kazi za Kibalozi zilizojitokeza huko nyuma.

viii) Kwa kuwa ni dhahiri Utalii wa Mikutano na matukio (business tourism) ni muhimu katika kuchangia na kukuza pato la Taifa kupitia Sekta ya Utalii, na kwa kuwa Vituo vyetu Vya Mikutano ya Kimataifa hususan kituo cha Arusha (AICC) havina Chombo Mahsusi (National Convention Bureau) cha kuitangaza Nchi na kuvutia Mikutano na maonesho ya Kitaifa kufanyika nchini, Serikali ione umuhimu wa kuanzisha Chombo hicho ili kuvutia Mikutano na Maonesho mengi ya Kimataifa kufanyika nchini na hatimaye kuongeza Pato la Taifa.

ix) Sambamba na ushauri uliotolewa hapo juu, ili kuimarisha Sekta ya Utalii nchini na kukuza pato la Taifa, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa kupitia Balozi

zake, iendelee kushirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii kutangaza utalii nje ya nchi ili watalii wengi zaidi watembelee Tanzania.

x) Kwa kuwa Serikali imekuwa na kasi ndogo ya ubadilishaji wa Sheria za Nchi ili kuendana na matakwa ya Itifaki ya Soko la pamoja la Afrika Mashariki, Serikali pamoja na Idara na Taasisi zake iongeze kasi ya ubadilishaji wa Sheria za Nchi zilizoainishwa ili ziendane na matakwa ya Itifaki ya Soko la Pamoja. Hii itawezesha Watanzania kunufaika ipasavyo na fursa za Soko la Pamoja la Afrika Mashariki na Jumuiya nyingine za Kikanda.

xi) Kwa kuwa ni dhahiri kuwa kuna uelewa mdogo miongoni mwa wananchi kuhusu masuala ya Mtangamano na faida zake, Serikali iendelee kutoa elimu kwa Umma kuhusu fursa zitokanazo na Jumuiya za Kikanda na Kimataifa ambazo Tanzania ni Mwanachama.

xii) Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuongeza kasi ya kuandaa Sera maalum kuhusu mtangamano wa Afrika Mashariki ili kuiwezesha Serikali kuwa na mwongozo wa kisera inapotekeleza masuala mbalimbali ya kijumuiya. Ushauri huu umekuwa ukitolewa mara kwa mara lakini haujazingatiwa kikamilifu.

xiii) Kwa mara nyingine tena, Kamati inaendelea kuisisitiza Serikali kukamilisha haraka upatikanaji wa Sera Mpya ya Mambo ya Nje. Kamati imekuwa ikishauri mara kwa mara kuhusu upatikanaji wa Sera Mpya ya Mambo ya Nje itakayoendana na hali ya sasa ya Diplomasia ya Uchumi lakini utekelezaji wake umeendelea kuchukua muda mrefu.

xiv) Serikali kwa kushirikiana na wadau wengine ijenge Chuo kipya cha Diplomasia cha kisasa Jijini Dodoma kitakachohamasisha nchi nyingine za Afrika na Duniani kwa ujumla kuleta wanafunzi wao na hatimaye kuongeza pato la Taifa kutokana na mapato yatokanayo na udahili wa wanafunzi hao. Aidha, ili kuvutia wanafunzi wengi zaidi, Chuo hiki kwa sasa kianze kufundisha lugha ya Kiswahili.

xv) Kamati inaendelea kuishauri Serikali kulipa michango yote ya Kimataifa na Mashirika yake ambayo nchi yetu inadaiwa hadi muda huu hususan ya "International Conference on the Great Lakes Region – ICGLR" ili kuendelea kujenga heshima ya muda mrefu ya nchi yetu mbele ya Jumuiya ya Kimataifa. Ushauri huu umekuwa ukitolewa mara kwa mara lakini haujazingatiwa kikamilifu;

xvi) Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuona umuhimu wa kuharakisha mchakato wa kupatikana kwa jengo la kisasa la Kurugenzi ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa upande wa Zanzibar;

xvii) Kamati imebaini kuwa bado vitendo vya unyanyasaji wa wafanyakazi wa majumbani kwa baadhi ya nchi za nje vinaendelea, hivyo Serikali iweke utaratibu utakaohakikisha kuwa panakuwepo na usalama wa Watanzania wanaofanya kazi mbalimbali nje ya nchi kabla na baada ya kuondoka nchini Tanzania;

xviii) Serikali iweke utaratibu mahsusi wa kufuatilia utekelezaji wa mikataba yenye tija kwa Taifa ambayo tumeingia na Serikali nyingine za Nchi za Nje. Hii itawezesha Tanzania kunufaika na

faida zitokanazo na mikataba hiyo ambayo baadhi yake imekuwa haitekelezwi kwa kasi inayostahili;

## SURA YA TANO

## HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha Taarifa hii. Napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha kukamilika kwa taarifa hii. Naomba niwatambue kwa majina kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Mussa Azzan Zungu, Mb, **Mwenyekiti**
2. Mhe. Salum Mwinyi Rehani, Mb, **M/Mwenyekiti**
3. Mhe. Shamsi Vuai Nahodha, Mb
4. Mhe. Mussa Hassan Mussa, Mb
5. Mhe. Prosper J. Mbena, Mb
6. Mhe. Victor Kilasile Mwambalasa, Mb
7. Mhe. Fakharia Shomari Khamis, Mb
8. Mhe. Cosato David Chumi, Mb
9. Mhe. Bonnah Mosses Kaluwa, Mb
10. Mhe. Masoud Abdallah Salim, Mb
11. Mhe. Sophia Hebron Mwakagenda, Mb
12. Mhe. Gerson Hosea Lwenge, Mb
13. Mhe. Shally Josepha Raymond, Mb
14. Mhe. Dkt. Suleiman Ally Yussuf, Mb
15. Mhe. Joram Ismael Hongoli, Mb
16. Mhe. Zacharia Paulo Issaay, Mb

17. Mhe. Joseph Michael Mkundi, Mb
18. Mhe. Mboni Mohamed Mhita, Mb
19. Mhe. Fatma Hassan Toufiq, Mb
20. Mhe. Sebastian Simon Kapufi, Mb
21. Mhe. Silafu Jumbe Maufi, Mb
22. Mhe. Ruth Hiyob Mollel, Mb
23. Mhe. Janeth Maurice Masaburi, Mb
24. Mhe. Augostino Manyanda Masele, Mb
25. Mhe. Almasi Athuman Maige, Mb

**Mheshimiwa Spika,** kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati napenda kutumia fursa hii kumshukuru Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki Mhe. Balozi Dkt. Augustine Philip Mahiga, (Mb), Naibu Waziri, Mhe. Dkt. Susan Alphonce Kolimba (Mb), Katibu Mkuu Prof. Adolf F. Mkenda, Naibu Katibu Mkuu Balozi Ramadhan Muombwa pamoja na Watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano na mchango wao katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu ya Kikanuni ya Kamati.

**Mheshimiwa Spika,** mwisho lakini si kwa umuhimu, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Stephen Kagaigai kwa kuratibu vema shughuli za Kamati na Bunge. Aidha, nawashukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Athumani Hussein, Mkurugenzi Msaidizi Bi. Angelina Sanga na Makatibu wa Kamati hii Ndg. Ramadhan Abdallah na Bi. Grace Bidya wakisaidiwa na Bi. Rehema Kimbe, kwa kuratibu vema shughuli za Kamati na kuhakikisha Taarifa hii inakamilika kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika

Mashariki kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

**Mheshimiwa Spika**, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

Mussa Azzan Zungu**, Mb**

**MWENYEKITI**

**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA**

23 Mei, 2018